



UTAFSIRI WA BIBLIA – updated 17-7-2017 by Abraham Kogo

I. Utanguliza wa jinsi ya kutafsiri Biblia

Hata ingawa sehemu nyingi kwa Biblia ni rahisi kuelewa, sehemu zingine sio rahizi kueleweka pila kusingatia maakizo za utafsiri wa Biblia. Tuna hitaji kujua utafsiri wa Biblia ili tujue maana ambaye mwandishi alikusudia. Sababu ya kusoma kuhusu utafsiri wa Biblia ni kwamba tuweze kufahamu kile ambacho mwandishi alimaanisha. Kwa mara nyingi tunakuwa na ugumu wa maana au lengo kuu wa mwandishi nahii imesababishwa na sababu kama kutoelewa lugha, wakati na mazingira ambamo mwandishi alikuwamo na ya leo. Utafsiri wa Biblia ni vile tunapojenga daraja kati ya mwandishi na sisi.

Wakristo wanakubaliana kwamba Biblia ni neno la Mungu. Wanaamini kwamba katika Biblia Mungu anazungumza nasi wazi kabisa na kuna utafsiri moja tu sahihi wa kila andiko katika Biblia. Huu ndio jambo ambao Mungu alimaanisha wakati aliwawezesha wanadamu kuandika maandiko. Kifungu kimoja kinaweza kuwa na mafundisho mengi, lakini maana ya kifungu hicho ni moja na maana hii ndio mwandishi ambaye alikuwa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu alimaanisha.

Kielelezo wa huu jambo inapatikana katika 2 Wakorintho 6:14. Maana la hili andiko ni kwamba atubaswi kushirikiana na wasio amini Kristo. Mkristo anawesa funga ndoa tu na Mkristo mwenzake, sisi Wakristo tunakataswa na Mungu kuoana na wasio amini. Jamno la pili ni kwamba Mkristo anakataswa kushiriki biashara na asiemwamini Mungu.

Je, tunawezaje kufahamu utafsiri kamili wa Biblia? Mafundisho ya Biblia kuhusu jinsi ya kutafsiri Biblia yatatusaidia sana kuhakikisha kwamba tunatafsiri Biblia kwa njia ambayo ukweli wa Biblia unajitokeza kwa wazi kabisa.

Ili tuweze kufahamu Biblia, ni lazima tufahamu wazi kabisa utafsiri wa Biblia. Mtume Paulo anasema kwamba, “Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli” (2 Timotheo 2:15). Hiki andiko inatuambia tusome Biblia ilituelewe na kuzingatia katika maisha yetu.

Kuna watu wengi wanao fikiria kwamba hakuna haja ya kusoma Biblia. Wanasema ya kwamba kazi yao tu ni kutegemea Roho Mtakatifu awafundishe. Huu ni kinyume na vile Biblia inatufundisha. Mbele na vile 2 Timoteo 2:15 inatufunza, Ezra 7:10 na Nehemia 8:13 wanaongea vile viongozi katika Agano la Kale walijifunza Biblia. Pia tukisoma kuhusu maisha ya Yesu kila wakati tunasoma kuhusu Yesu akifunsa wafuasi

wake. Ukitaka kujua kuhusu Yesu, ni lazima usome Bibilia na ni lazima uweke wakati mwingi na jukumu la kusoma.

Kusudi la mafundisho haya ni kuonyesha baadhi ya kanuni za kutafsiri Bibilia.

II. Mambo ambayo tunapaswa kukumbuka kuhusu Bibilia.

1. Kufahamu au kutafsiri Bibilia.

A. Mtume Petro aliwakumbusha wasomaji wake kwamba kuna mambo mengi katika maandishi ya Paulo ambayo yalikuwa magumu kuelewa (2 Petro 3:15-16).

B. Kuna kurasa kadhaa wa kadhaa katika Bibilia ambazo hatuelewi kwa wazi kabisa. Mfano ni Mwanzo 6:2. Harufahamu kabisa wana wa Mungu hapa ni kina nani. Jambo lingine gumu la kuelewa linapatikana katika Kutoka 28:30 ambapo tunasoma kuhusu “Urim na Thummim.” Tunaona maneno haya mara kwa mara katika Agano la Kale na hatuyaelewi kabisa.

C. Mambo ya muhimu ya Bibilia tunaweza kuyafahamu vyema kabisa kwa sababu yamerudiwa rudiwa mara kwa mara. Kumbu Kumbu la Torati 29:29 na Isahia 55:8-9, yatufunza kuwa Mungu haja dhahirisha kila jambo kwetu sisi na anayefikiria sio vile tuafyo fikiria.

i. Kila mtu anaweza kufahamu kurasa fulani katika Bibilia, hata wale ambao hawajaokoka. Lakini ukweli ni kwamba kuna mambo mengi ambao hayawezi kueleweka na wale ambao hawajaokoka. Hii ni kwa sababu Roho Mtakatifu ndiye anatusaidia kufahamu Bibilia na kuitii. Epeso 3:5 na 1 Wakorintho 2:14, inafundisha kwamba tunahitaji Roho Mtakatifu ili tuweze kufahamu Bibilia vyema.

ii. Wale ambao hawajaokoka hawawezi kufahamu Bibilia kwa sababu Roho Mtakatifu ambaye anatuwezesha kufahamu Bibilia, haishi ndani mwao. Soma 1 Wakorintho 1:18 mahala ambapo Paulo alisema neno la msalaba ni ubumbafu kwa walio potea.

2. Bibilia ni neno la Mungu.

A. Bibilia ni neno la Mungu (2 Timotheo.3:16) na ni mapenzi ya Mungu kwamba leo tuwe na Bibilia ambayo imeandikwa. Wanadamu walizungumza na kuandika Bibilia wakiwa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu (2 Petero 1: 20-21).

B. Wakristo wanaamini kwamba Bibilia ni ukweli kutoka kwa Mungu, na kwa hivyo Bibilia ina mamlaka na haina makosa yoyote na inatosheleza kwa maagizo. Lazima tukubali na kuzingatia maakizo za Bibilia. Amri hizi zinatoka kw Mungu mwenyewe. Ni lazima Mkristo akubali na kutii kila fundisho kwa Bibilia. Kama atukubali hata amri moja atutaweza kukubali Imani yoyote ya Bibilia. Sisi tukiwa wanadamu hatuwezi chakua chenye tunataka kuamini. Mungu pekee yake ndiye anaweza kutuchakua na ametuonyesha jambo hili kwa kuchakua Bibilia.

C. Biblia ni neno la Mungu. Wanadamu waliandika Biblia katika lugha ambazo walifahamu vyema na kwa njia ambayo walielewa kuandika. Lakini walipokuwa wanaandika, walielezwa ya kuandika na Roho Mtakatifu.

i. Hii inamaansa kwamba wao walizungumza na kuandika maneno ya Mungu. Kile ambacho walisema, hakikutokana na mawazo yao, wao walikuwa chombo. Ukweli ambao waliandika ulikuwa ukweli wa Mungu. Maana ya ukweli huu, ilikuwa maana kuitoka kwa Mungu. Mungu anazungumza ujumbe wake kupitia kwa waandishi ambao ni wanadamu.

ii. Wakati walipokuwa wanaandika, waliongozwa na Mungu. Mungu hakuwapa tu ukweli na kuwaacha wauzungumze kwa njia yao wenyewe. Petro anasema kwamba kwa kila sehemu walipokuwa wanazungumza ukweli huo, Roho Mtakatifu ndiye aliyewaongoza (2 Petro 1:21).

iii. Maana ya hii ni kwamba wakati walipokuwa wanaandika, walichagua maneno ambayo Mungu mwenyewe aliyaweka katika mawazo na vinywa zao. Kwa njia hii maneno ta wale ambao waliandika Biblia, yalikuwa maneno ya Mungu mwenyewe.

iv. Paulo anafundisha kwamba Biblia ni neno la Mungu na lafaa kwa kufundisha. 2 Timotheo 3:16, Biblia yote; Agano la Kale na Agano Jipya ni neno la Mungu ambalo liliandikwa na wanadamu walipokuwa wanaongozwa na Roho Mtakatifu.

Mambo yote tunayojua kuhusu Mungu linapatikana kwa Biblia. Kumbuka huu amri wa maana. Usikubali mambo unayoyasikia mtu husema kumuhusu Mungu bali uyachunguze kama yasemwapo inapatikana kwa Biblia.

3. Biblia haina makossa yoyote.

A. Katika lugha ambayo Biblia iliandikwa, hakukuwa na makossa.

B. Biblia zetu za sasa huenda ni tofauti lakini ujumbe ni ule ule. Mungu ameulinda ujumbe wa Biblia. Kuna makossa madogo ambayo yalisababishwa na jinsi ujumbe huo ulivyokuwa umewekwa. Kwa mfano:

2 Samueli 10:18 tunasoma kuhusu magari ya farasi 700 na katika 1 Mambo ya Nyakati 19:18 tunasoma kuhusu magari ya farasi 7,000.

2 Wafalme 24:8 Mfalme alikuwa na miaka 18 na katika 2 Mambo ya Nyakati 36:9 tunasoma kwamba alikuwa miaka 8.

1 Wafalme 4:26 na 2 Mambo ya Nyakati 9: 25, kuna utofauti wa idadi ya farasi.

C. Tafsiri za Biblia ambazo ni nzuri: KJV; ESV na NASB. Tafsiri hizi zimetafsiriwa kutoka kwa tafsiri za kwanza kabisa katika lugha ambazo ziko na zimetafsiriwa vilivyo.

D. Kuna tafsiri za uongo ambazo zimetafsiriwa na kusudi ya kupotosha wasomaji wa tafsiri hizo. Epuka na tafsiri kama hizo. Moja wa hizi tafsiri ni “New world Translation” (Utafsiri wa Ulimwengu Upya) ambaye ni ya mashahidi wa Yehova na

kitabu cha Mormoni. Wamepadhilisha Biblia ili waifanye mafundisho yao ya uonge ikubalike.

i. Angalia tofauti kati ya Biblia Takatifu na Mashahidi wa Yehova:

Yohana 1:1 kutoka Biblia Takatifu ina sema ya kwamba: Hapo mwanzo Mungu alikuwa Neno na Neno alikuwa na Mungu na Neno ilikuwa Mungu

Mafundisho ya uongo kutoka Mashahidi wa Yehova wameongeza hili neno na husema “Hapo mwanzo kulikuwa Neno, na Neno alikuwa na Mungu, na Neno ilikuwa ni mungu (herufi ndogo). Kuongesa neno “ni” imebadhili maana andiko. Maana kuu katika Biblia ni kwamba Yesu ni Mungu ambaye amekuwa mmoja katika Utatu

Mashahidi wa Yehova awaamini kwamba Yesu ni Bwana na pia awaamini katika Utatu. Kwa kuiweka neno “ni” katika sentensi uifanya Yesu kuwa kama Malaika lakini sio Mungu Mkuu.

E. Tafsiri ya hivi karibuni ya NIV pia hapaswi kusomwa kwa sababu imebadilisha maneno mengi kama “uume” (he or him) liwe “awa” (they or them). Chunguza chapisho lako kwa sababu mengi yamechapishwa hivi karibuni. Chapisho la NIV ya 1984 ni tafsiri nzuri sana. Usiamini chapisho ya hivi punde.

4. Umoja wa Biblia: Biblia ina vitabu 66, ambavyo vimeandikwa na zaid ya watu 40 ambao wanatoka sehemu tofauti tofauti, kiwango cha masoma tofauti na kwa wakati tofauti kwa zaidi ya miaka 1600. Lakini biblia ni kitabu kimoja. Hii ni kwa sababu Mungu ndiye mwandishi mkuu wa Biblia.

5. Kristo Yesu ndiye ujumbe wa biblia. Agano la Kale linatazamia kuja kwa Kristo na Agano Jipya linahusu kuja kwa Kristo.

Utafsiri wa Biblia unahusu kanuni na mtindo fulani fulani. Hii inajumlisha kufahamu maana ya kifungu na jinsi kinavyotuzungumzia leo. Utafsiri wa Biblia maana yake ni kujaribu kuelewa mwandishi katika nyakati ambamo aliandika na jinsi maandishio hayo yanavyotungumzia leo.

- A. Sababu kuu ya kazi hii ya utafsiri ni kujua maana ya mwandishi alipokuwa anaandika na maana ya leo kwetu. Kuna amri ambazo zimepeanwa katika Agano la Kale ambazo hazifanyi kazi leo. Kwa mfano kula nguruwe.
- B. Kuna aina tatu za amri katika Agano la Kale . Moja kati ya hizi tatu inazingatiwa na waumini.
 - i. Moja ya hizi amri ni ile amri ya taifa la Israeli. Hii ni amri iliyoilinda inji ya Israeli katika Biblia. Inji ya Israeli na ufalme wake haikukaa mbaka wa leo ivyo basi hayo amri ya taif ya Israeli aina maana leo.
 - ii. Aina ya pili ni amri ya sherehe ambaye hatuazingatii tena. Mfano ni umwakigaji wa damu ya wanyama. Hebrania 10:10-14 inatufunza Yesu ndie tabiu wa kweli na wa mwisho. Hakuna tabiu mwingine tena.
 - iii. Amri wa tatu ni amri kumi za Mungu ambayo inazingatiwa na Wakristo wote.

6. Biblia ina mamlaka.

A. Biblia ilitoka kwa Mungu; kwa sababu hii, tunafaa kutii yote bali tu iwapo Biblia enyewe inatambua tusitii jambo vulani kama vile tunaeswa katika Matendo ya Mitume 10:9-16 inayetuambia kwamba chakula yote inakulwa.

II. Kwa nini tunahitaji utafisiri wa Biblia?

1. Jambo hili ni muhimu kwa sababu hatuishi katika nyakati za wale ambao waliandika Biblia. Picha tunaoangazia ni juwa waandishi wa Biblia wako kwa mto ngambo ile wala sisi tuko ngambo ingine. Utafsiri wa Biblia ni kama vile tunaiweka daraja kwa mto ili neno halali ya Biblia lipate kutufikia hili tuielewe vilivyo kusudiwa.

Kuna mambo ambayo wale ambao waliandika walielewa, lakini leo hatuyaelewi. Kwa mfano “Urim na Thummim” waandishi wa wakati huo walielewa vyema sana. Tunaona maneno haya mara kwa mara katika Agano la Kale. Kutoka 28:30 na Hesabu 27:21. Mambo ambayo hatuyaelewi sana si ya msingi katika Biblia.

A. Kuwa mwangalifu usimwamini mtu ambaye anasema kwamba anajua kila kitu cha Biblia.

III. Mambo ambayo tunafaa kuzingatia ya kawaida katika utafsiri wa Biblia.

1. Umuhimu wa kuchunguza vyema. Tazama Luka 17:21, “..tazama ufalme wa Mungu umo ndani yenu.”

A. Tazama kifungu vyema na uulize na ujibu maswali haya:

- i. Je, ni nani ambaye alikuwa anazungumza? Yesu ndiye alikuwa anazungumza.
- ii. Je, ni kwa nini alikuwa anazungumza? Yeye alikuwa anajibu swali.
- iii. Ni swali gani ambalo alikuwa analijibu? Je, ufalme wa Mungu utakuja wakati gani.
- iv. Je, nani maybe aliuliza swali hili? Mafarisayo.
- v. Je, Mafarisayo walikuwa kina nani? Wao walikundi kikundi cha dini ambacho kilimpinga sana Kristo.
- vi. Je, Yesu alikuwa nani? Yeye alikuwa Mwana wa Mungu ambaye ni Mesiya. Yeye ndiye Mfalme wa wafalme.

B. Kwa kutumia maswali kama haya na mengine, tunaweza kupata utafsiri wa Biblia vyema. Tunajua kwamba hawa Mafarisayo hawakuwa wakristo kwa sababu hii tunajua kwamba Ufalme haukuwa ndani mwao. Tunajua kwamba Yesu ndiye Mfalme wa Ufalme ambaye alikuwa anaishi miongoni mwao.

C. Utumiaji wa maneno sawa ni jambo la muhimu sana. Masadukayo hawakuamini katika maisha baada ya kifo. Katika Mathayo 22:29-32, Yesu alisema Yeye si Mungu

wa wale ambao wamekufa. Alitumia walio badala ya ambao kuonyesha kwamba Abrahamu, Isaka na Yakobo wako hai.

D. Chukua muda wako kusoma kifungu. Soma mara kwa mara. Soma, omba, tafakari na urudie ili uelewe Bibilia. Bibilia mara kwa mara udahirisha maan pole pole kila wakati. Mimi ni mzee na kila wakati nikizoma Bibilia ninatasama na kuilewa mambo mabya katika kila mstari.

E. Mfano mwingine hi huu: Yohana 5:24, Yesu anasema, Amini, amini, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna na uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.

i. Je, maneno ya muhimu hapa ni gani? Amini, amini, uzima wa milele, hukumuni na mautini.

ii. Je, maneno haya yanaingianaje? Yesu anatumia neno, wala, kuonyesha uhusiano kati ya kifo na uzima.

iii. Je, ni nani ambaye anazungumza? Yesu ndiye anazungumza.

iv. Je, Yesu anazungumza na nani? Anazungumza na Wayahudi.

v. Je, tabia ya waliokuwa wanamsikiliza ni gani? Wayahudi walikuwa wanapanga kumwua.

vi. Je ni jambo gani ambalo tunaona kuhusu maneno ambayo yametumika hapa? Maneno haya yanaonyesha kwamba mara tu mtu anapoamini, yeye anapata uzima wa milele.

F. Utafsiri wa kweli ni kwamba Yesu Kristo alikuwa na jambo la muhimu sana mablo alitaka kuwaeleza watu. Anasema kwamba uzima wa milele si jambo ambalo linatapatikana baadaye, bali ni kitu ambacho ambacho kinapatikana sasa. Umuhimu wa mstari ni kwamba alikuwa anazungumza tofauti ya uzima wa milele na kifo cha milele. Anasema kwamba yule ambaye ameokoka, amesamehewa dhambi zake na ataisha maisha yake ya milele huko mbinguni.

2. Je, ni nani ambaye aliandika kifungu na kifungu hiki kimeelezwa nani? Je sababu ya kifungu hiki ni gani?

A. Ni jambo la muhimu kufahamu mwandishi wa kifungu fulani, maisha yake na mazingira ambao alikuwa anaishi na yalishawishi uandishi wake. Jambo la muhimu pia kwamba tunapaswa kufahamu kwa wazi kabisa kusudi la mwandishi na mpango wake katika kuandika kifungu kitabu fulani. Kwa mfano, Katika Yohana 20:31, Yohana anaeleza sababu yake ya kuandika Injili yake, “haya yameandikwa ili mpate kuamini kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu na kwamba kwa kuamini, mpate kupata uzima wa milele ndani Mwake.” Kusudi hili Yohana analiweka wazi kabisa. Mara kwa mara huwa si jambo rahisi kufahamu kusudi la mwandishi. Mambo yafuatayo yanaweza kukusaidia kufahamu kusudi na mpango wa mwandishi.

B. Tafuta uone kama kusudi limeelezwa au la. Ikiwa kusudi hilo halijaelezwwa, je kuna mambo ambayo yanaonyesha kwamba kuna kusudi hilo? Kwa mfano katika barua za Paulo kwa kanisa la Wakorintho, haeleza kamwe kusudi kwa wazi kabisa. Lakinit uanweza kutafuta kusudi hilo kwa kutazama 1 Wakorintho 1:11, 3:3-4, 4:6, 5:6. Kutokana na mistari hii tunasoma kwamba kulikuwa na mambo ambayo yalihatijika kusuluhishwa katika kanisa. Kulikuwa na wale ambao walikuwa wanapinga katika ya Paulo kama mtume. Paulo aliandika ili kutatua jambo hilo.

C. Mambo ambayo yananukuliwa kwa mwandishi huwa yanasaidia kudhihirisha kusudi la kitabu. Maada au vichwa ambavyo vinarudiwa rudiwa huwa pia ni njia ya kusaidia kujua kusudi na mpango wa mwandishi. Mathayo aliandika kitabu chake kutueleza kuhusu Ufalme wa mbinguni kwa sababu hili jambo ambalo anarudia mara kwa mara.

D. Tazama mfumo wa uandishi wa kitabu kama kuna jisni kitabu kimegawanywa katika sehemu tofauti tofauti.

E. Wakati kusudi na mpango umewekwa wazi kabisa, basi ni lazima tusoma kila sehemu ya kitabu hicho kusudi na mpango ukiwa ndio unatuelekeza. Hakikisha kwamba utafsiri wako unaambatana na kusudi na mpango wa kitabu hicho.

Mfano mwema ni Wafilipi 2:1-8. Tunaona kusudi la mwandishi. Maneno kama kuweni na nia moja, upendo, yanadhihirisha kwamba Paulo alijali sana ushirika katika kanisa la Filipi. Kwa sababu hiyo katika mistari ta 5-8, anawakumbusha kuhusu mfano mkuu wa Kristo. Kristo alifanya mambo fulani kwa sababu aliwaza kwa njia mzuri.

3. Je, kifungu kinasema nini kwa nmaneno rahisi sana?

A. Unapokuwa unasoma kifungu kutoka kwa Biblia, ni jambo jema sana kuona kifungu hicho kama mazungumzo kati yako mna mwandishi. Kwa sababu hii, msomaji unapaswa kuhakikisha kwamba unafahamu kusudi na mpango wa mwandishi. Kumbuka kwamba kuna moja moja kuu ya kifungu.

B. Mambo mingi katika Biblia si magumu kuelewa na kwa hivyo usiyafanya kuwa magumu.

C. Chunguza maana ya maneno katika lugha ambayo mwandishi aliandika na uhakikishe kwamba unafahamu maana yake leo. Ni jambo la muhimu sana kufahamu kwanza msomaji wa kwanza alifahamu maneno haya aje. Halafu tunapaswa kulinganisha maneno halisi ya kwanza na jinsi tunavyofahamu leo.

i Kwa mfano wakati Paulo aliandika barua kwa wakolosai, aliandiaka akitaka kuwaonya kuhusu walimui wa uongo wakati huo. Kwa sababu alitumia maneno ambayo yalitumika na hawa walimu wa wakati huo. Kwa mfano yeye alitumia neno siri katika wakolosai 1:25-26. Hili ni neno ambalo lilitumiwa na hawa waliwa wa uongo wakimaanisha mambo ambayo yalifahamika kwa wachache tu. Paulo anatumia neno hili kwa waeleza maana halisi ya neno hili, ambayo ni mpango wa Mungu wa wokovu ambao haukujulikana hapo mbeleni lakini sasa umefunuliwa kupitia kwa

Kristo Yesu. Jina la Yesu halikujulina katika Agano la Kale. Lakini sasa tunajua kwamba hili ndilo Jina ambalo linaokoa.

4. Kabla ya kufahamu maana ya kifungu, ni vyema kutazama maneno yake kuona kama kifungu hiki kina mafundisho kwetu leo. Kumbuka kwamba si kila kina mafundisho kwetu leo kama Walawi 11:7.

A. Kuna vifungu ambavyo havina mafundisho kwetu leo. Kwa mfano sheria za sherehe ambazo zinahusu kuabudu kwa Israeli kama maagizo kwa hekalu, kazi ya makuhani na jisni ya kutoa sadaka.

B. Wakati maana ya maneno ya hapo mwanzoni, yanafundisho tofauti kwetu leo. Kwa mfano ni kama Petro anapowauliza washirika wa kanisa kusalimiana kwa busu la upendo (1 Petro 5:14). Leo ujumbe ni kusalimia kwa njia ya upendo.

i. Pia ni jambo muhimu sana kutazama maneno ambayo yanamafundisho kwa msomaji wa kwanza n ahata kwetu leo bila kuyabadilisha. Haya yanaistwa maneo ya hakika. Kwa mfano Mungu anachukia usenge katika Warumi 1:27. Mungu alichukia dhambi vibaya sana katika Agano la Kale kama tu vile anachukia hata leo.

ii. Tunapaswa kuwa waangalifu sana kwamba tusije tukawa watu wa kufuta tu sheria. Kwa mfani ni kama wakati Kristo aliwaonsha wanafunzi wake miguu. Leo hatujamrisha kuoshana miguu.

C. Je, kifungu hiki kinafundisha nini hapo na hapo? Hii inamaansiah jinsi maneno yanavyotumika. Maneno mengi katika ligha ya kinegereza yana maana tofauti tofauti kulingana na jinsi yanavyotumika.

5. Jinsi unavyofikia uamuzi katika kusoma kwako.

A. Je, ninafiaje uamuzi kuhusu kifungu fulani? Kuwa mwangalifu sana kutofanya uamuzi mbaya. Je, uamuzi wangu unakubaliana au unakosa kukubaliana na maandiko ya Biblia na wengine ambao wamesoma kifungu hiki?

B. Je, wengine wametafsiri kifungu hiki kwa njia gani?

C. Je, nimejifunza nini na ninawezaje kuishi maisha yangu kulingana na ale ambayo nimeyasoma?

D. Kumbuka kwamba Biblia haina makossa yoyote. Ikiwa unawaza kwamba umepata mahali ambao kuna makossa, fahamu kwamba ni wewe mwenye makossa na wala si Biblia.

6. Umuhimu wa kufahamu kile ambacho kinafundishwa. Hili ni la muhimu kwa sababu unadhihirisha umuhimu wa maneno ambayo yametumika.

A. Kwa mfano ni neno kimbiba. Mtoto anakimbia shuleni. Raisi anakimbia au anawania kuwa raisi. Neno hili linamaana mara mbili kulingana na jisni linavyotumika.

B. Mfano mwingine ni utumiaji wa neno kulala katika Biblia. Linamaana ya kulala katika Mathayo 28:13 na pia linamaana na kufa katika 1 Wathesalonike 4:14.

7. Kuna utumiaji wa maneno wa aina mbili ambao tunapaswa kuangazia sana katika Biblia. Kuna utumiaji wa maneno katika historia na utumiaji wa maneno kwa kawaida.

A. Utumiaji wa maneno katika historia

Mara kwa mara ni jambo muhimu kufahamu historia ya kifungu na kuelewa maana kifungu hicho.

i. Mfano mzuri ni hadithi ya msamari mwema katika Luka 10:25-37. Tunajua kwamba Wayahudi waliwachukia sana Wasamaria. Waliwachukia sana kwa sababu baada ya taifa la Isreali la kasikazini kuondolewa katika nchi yao na Washuru, Wasamaria waliletwa humo. Tunapofahamu hili, basi historia inakuwa ya maana kwetu.

Tunafundishwa kuhusu upendo wa kindugu ambao Biblia inafundisha kwa tunapaswa kuwa nao kwa majirani wetu (Walawi 19:18). Tunaposoma hadithi katika Luka, tunaona kwamba wayahudi wawili ambao walikuwa watu dini wakimpuuza yule ambaye alikuwa ameumizwa. Lakini msamaria ambaye alikuwa amedharauliwa na Wayahudi alimsaidia yule ambaye alikuwa ameumizwa. Je, ni nani ambaye alikuwa mtiifu kwa Mungu?

Kwa sababu sasa tunafahamu historia ya kifungu, tunapaswa kuona tunajinza nini kutokana na kifungu hiki. Funzo ambalo tunalipata leo ni kwamba tunapaswa kuwa majirani wenye upendo na kuwasaidia hata kama wao ni kabira lingine.

B. Utumiaji wa maneno kwa kawaida.

Jambo linatusaidi pia kufahamu maana ya kifungu. Tunaweza kubadilisha maana ya neno ikiwa tutalitumia kinyume na mafundisho ya kifungu. Mtu ambaye anataka kuoa anaweza kutumia maneno yafuatayo kwa njia ambayo anataka kwa sababu anatakuoa.

i. Sehemu ya mwisho ya 1 Wakorintho 7:36, inasema kwamba wacha wao waoleke au waoe.

ii. Yohana 13:27, inasema kwamba kile ambacho unataka kufanya, fanya kwa haraka.

iii. Usije ukatumia mistari hii miwili kwa sababu unataka kuoa kwa haraka sana. Mistari hii miwili haihusiki kamwe.

C. Zingatia sana mistari mingine katika kifungu hicho ili uweze kufahamu maana halisi ya kifungu au mistari. Kwa mfano, kuna wale ambao wanawaza kwamba kufunga uzazi ni dhambi kwa sababu ya kusoma Mwanzo 1:28 bila kuzingatia mistari ambayo inatungulia mistari huu.

i. Mwanzo 1:26-28, Mungu akasema, Tumwumbe mwanadamu katika mfano wetu. Na atawale juu ya samaki wa majini na juu ya ndege za agani na juu ya wanyama na juu ya nchi na chohcote kitambacho aridhini. Mungu akamwumba mwanadamu katika mfano wake. Mungu akawabariki na kuwaambia, Mzae na mwongezeke na

mwitawale dunia na mtawale juu ya samaki wa majini, juu ya ndege wa angani na juu kile kitu kitambacho aridhini. Mungu alikuwa anawaambia watu wawili kwamba waitawale dunia. Ukweli ni kwamba walihitaji watu wengi ili wawasaidie kutawala dunia na kwa sababu Mungu aliwaambia wajijaze dunai. Leo tuna watu 7,000,000,000, kumanisha kwamba tumetii amri hii.

D. Ni hatari ya kupuuza jinsi neno linatumika kwa kawaida. Mtu anaweza kutumia Biblia kwa njia yoyote ambayo anataka. Hivi ndivyo walimu wa uongo huwa wanafanya.

E. Kupuuza jinsi neno limetumika katika mazingira itasababisha kutafsiri Biblia vibaya. Tutazame mifano miwili:

i. Wakati mwingine watu hutumia neno vibaya kudhihirisha jambo ambalo Biblia haifundishi kamwe. Watu hawa wanataka Biblia iseme jambo ambalo wanataka na kwa sababu hii wanatumia mistari na vifungu vya Biblia vibaya.

ii. Kwa mfano watu ambao wanataka kudhihirisha kwamba Biblia inakataza unywaji pombe, wao hutumia Luka 1:15. Hili ni jambo bay asana kwa sababu katika mstari wa 13, Malaika alikuwa anampa maagizo baba ya Yohana Mbatizaji. Biblia haikataza utumiaji pombe lakini inakataza ulevi. Kuna vifungu katika Biblia ambavyo kwa wazi kabisa vinafundisha kuhusu pombe (Warumi 14:13).

iii. Kuna wale ambao pia wanatumia Luka 10:9 kusema kwamba tunauwezo wa kuwaponya wengine na kwamba wakristo wako na nguvu za ajabu. Katika Luka 10:-119, tunasoma kwamba Yesu aliwapaa wale 72 nguvu za kipekee wakati aliwatuma waende kuhubiri Injili.

IV. Mambo ambayo tunapaswa kuzingatia sana wakati tunafanya utafsiri wa Biblia.

1. Maisha ya mwandishi na jinsi maisha yake yanashawishi uandishi wake.

Maisha ya mwandishi huwa mara kwa mara yanadhihirisha maana ya kifungu fulani. Maandishi mengi huwa yanabadilika wakati tunapozingatia maisha na hali ya mwandishi.

A. Mfano mzuri ni Zaburi 51 ambayo iliandikwa na Daudi baada ya kuanguka dhambi na Bethsheba na kumwua Uraya ambaye alikuwa mume wa Bethsheba. Daudi aliandika Zaburi akiwa anatubu na kukiri dhambi yake na kuomba msamaha. Zaburi inatufundisha kuhusu toba.

2. Tunapaswa kufahamu historia ya Agano la Kale ikiwa tutafahamu Agano Jipya. Hatuwezi kamwe kufahamu kitabu cha Waebrania ikiwa hatufahamu Agano la Kale.

A. Yesu alinukuu sana Agano la Kale alipokuwa anafundisha. Mara kwa mara tunaweza kutumia kifungu cha Agano la Kale kutafsiri Agano Jipya. Kwa mfano, Yesu alizungumzia Hesabu 21:4-9, wakati alipomwambia Nikodemo, kama tu vile Musa alivyomwinua nyoka wa shaba jangwani, vivyo hivyo, Mwana wa Adamu lazima ainuliwe juu pia. Kutokana na kufahamu historia ya Agano la Kale, tunaona

kufanana kwa vifungu hivi. Wayahudi walielezwa wamtazame Mungu kwa ajili ya msamaha na ukombozi kama tu vile tunavyomtazama Kristo kwa ajili ya msamaha wa dhambi.

3. Vitabu vya historia na jiografia, ni vizuri kwa sababu vinatusaidia katika kufahamu mafundisho ya kifungu. Kwa mfano maono ya Danieli katika Danieli 2:31-45. Tunasoma kuhusu tawala nne kuu ambazo ni Babeli, Persia, Ugiriki na Roma ambazo zingegangamia baadaye. Vitabu vya historia vinatufundisha mengi kuhusu tawala hizi na kutusaidia kufahamu Biblia vyema. Kwa mfano kufahamu historia ya Warumi, hutusaia kufahamu kwa watosza ushuru kama Mathayo walikuwa wamedharauliwa sana na kuchukiwa. Sababu ni kwamba wao walikuwa watu wakuchukua rushwa na wenye tamaa.

A. Mara nyingi, kuelewa mengi kuhusu jiografia itakusaidia kufahamu maana ya kifungu. Kwa mfano, Yesu alianza mfano wa Msamaria mwema kwa kusema, mtu mmoja likuwa anaenda Yerusalemu akitoka Yeriko..(Luka 10:30). Tunajua kwamba nchi hii ilikuwa na milima ambayo iliawezesha wezi kuwavamia na kuwapora watu.

B. Kufahamu hali ya maisha pia hutuwezesha kufahamu vifungu kama Waefeso 5:21-6:9. Kwa mfano unahitaji kufahamu jambo kuhusu kya za kirumi ikiwa utafahamu mafundisho ya kifungu hiki. Mafundisho haya yalikuwa yawasaidie wakristo katika maisha yao ya nyumbani. Kanuni na tamaduni za wakati huo ziliwafanya waume kuwalazimisha wake wao kutii lakini hazikueleza kwamba waume walipaswa kuwapenda wake wao. Katiika Waefeso 5:25-31, Paulo anafundisha kwamba waume wana jukumu la kuwalida na kuwapenda wake wao.

C. Hali ya uchumi pia ni jambo lingine ambalo litakusaidia pia kufahamu kifungu fulani. Ikiwa tutafahamu kwamba wengi wa wakristo katika Biblia walikuwa watu maskini, tutafahamu kwamba tunapaswa kutoa kwa kujitolea. 1 Mambo ya Nyakati 29 na 2 Wakorintho 8, tunasoma kwamba wakristo ambao walikuwa maskini walitoa kwa kujitolea. Huu ni mfano mkuu sana kwetu leo.

D. Pia ni jambo la muhimu kufahamu sheria za wakati huo. Matendo ya Mitume 16:37-39, tunasoma kwamba Paulo alikuwa mwenye wa taifa la Roma na kwa hivyo alikuwa na haki kama mwenyeweji. Sheria ya Roma ilimlinda kutokana na kupingwa na ilimkubali kukata rufu kwa Kaisari ili kesi yake isikilizwe huko Roma.

E. Kufahamu mambo haya mara kwa mara hutusaidia kufahamu Biblia vyema kabisa. Mfano wa hii unapatikana katika Zaburi 23 ambayo ni zaburi nzuri ya kuwafariji wakristo. Tunasoma kwamba mchungaji anachunga kondoo zake vizuri sana. Kutokana nah ii tunaona kwamba Bwana Yesu anawachunga watu wake vizuri sana. Yeye huwa anatuongoza na kutulinda. Hatufai kuogopa lolote kwa sababu Kristo Yesu mchungaji wetu yupo nasi kila wakati.

V. Maana na jinsi ya kuishi maisha yetu kulingana na mafundisho ya kifungu.

1. Je, ni mwandishi ambaye anaamua kifungu kinamaanisha nini? Kuna wale ambao wanawaza kwamba ni msomaji ambaye anapaswa kuamua maana ya kifungu. Lakini ikiwa unaamini kwamba Biblia ni neno la Mungu, na kwamba Mungu amepema

Biblia ili atuongoze, basi tunapaswa kuisoma tukijiuliza ni nini ambacho Mungu anasema katika kifungu.

A. Mojawapo wa kanuni za kutafsiri Biblia ni kwamba hatajitafutii maana ya kifungu. Bali tunapaswa kukubali maana ya kifungu ambacho mwandishi ameandika. Lengo letu ni kujua maana ambayo Mungu anamaanisha katika kifungu ambacho tunakisoma.

2. Tunapaswa kutambua maana ya neno na jinsi tunapaswa kuishi maisha yetu kulingana na maana hiyo.

A. Manaa ya kifungu ndio mwandishi alikusudia wakati alaiipoandika kifungu hicho. Maana ya kifungu inataoka kwa mwandishi.

i. Kwa mfano ni jinsi Mungu anataka tuje kwake. Tunaweza tu kuja kwa Mungu kupitia kwa Kristo Yesu. Hili ndilo kusudi la mwandishi katika Yohana 14:6.

ii. Kuna wale ambao wanasoma hili ni kusema kwamba msomaji ana uhuru wa kufahamu kifungu jinsi anataka kukifahamu. Kuna watu na madhehebu ambao wanafahamu Yohana 14:6 vibaya. Wanasema kwamba Mungu wao ni mkubwa na kwamba Mungu atawakubali wale ambao ni wazuri kuingia mbinguni bila kupitia kwa Yesu Kristo. Huu ni uongo.

B. Tunapofahamu maana ya kifungu ndipo tutaweza kuishi maisha yetu kulingana na kifungu hicho. Kile tunapaswa kufanya na Yohana 14:6, ni kuhakikishi kwamba tunakuja kwa Kristo ikiwa tunataka kuingia mbinguni. Bila Kristo hakuna kuingia mbinguni.

3. Kuishi maisha yako kulinagana na mafundisho ya Biblia.

A. Huwezi kuishi maisha yako kulingana na mafundisho ya Biblia ikiwa unajua kile ambacho Biblia inakifundisha. Kujua kile ambacho Mungu anataka kwetu na kukosa kuishi hivyo ni bure.

i. Kwa mfano, katika Mathayo 28:18-20, ikiwa amri hii tungekuwa tumetii kikamilifu, injili ingekuwa imefika ulimwenguni kote. Lakini unapotazama ni kwamba injili haijafika kila mahali. Kuna wengi leo ambao wamepata masomo ya chuo kikuonya Biblia ambao wanataka tu kufurahia maisha mazuri ya humu duniani.

VI. Kuelewa Agano la Kale

1. Kuna hatua tano za muhimu katika kutafsiri Agano la Kale. Hatua hizi hazitumika katika kila kifungu.

A. Kwanza, kufahamu maana ya kifungu kwa wasilikizaji wa kwanza.

B. Je, tofauti ni gani katika wasikilizaji wa Agano la Kale na sisi leo?

C. Je, kanuni ya kifungu ni gani?

D. Je, Agano Jipya linabadilisha kanuni? Kwa mfano kama kula nguruwe.

E. Je, tunawezaji kuishi maisha yetu leo kulinagana na mafundisho ya kifungu?

2. Vitabu vya sheria.

A. Vitabu vya sheria ni baadhi ya historia ya taifa la Israeli.

B. Sheria inapeanwa katika mazingira ya Agano lijulikanalo kama Agano la Musa (Kutoka 19:24).

C. Tutafsiri Agano la Musa.

i. Ndipo watu wa Israeli wabarikiwa, walihitaji kutii Mungu.

ii. Agano Jipya limechukua na nafasi ya Agano la Musa.

iii. Kuna mafundisho ya Agano la Kale ambayo tunapaswa kufuata ikiwa tutayazingati katika ukweli wa Agano Jipya.

iv. Tunaposoma Agano Jipya tunaona kwamba hatupaswi kufuata sheria za sherehe, lakini sheria za madili bado tunafaa kuzitii. Sasa tunaweza kula nguruwe na pia tutii amri kumi za Mungu.

3. Unabii wa Agano la Kale kuna wakati unaeleweka kwa rahisi na wakati mwingine unakuwa mgumu kufahamu kabisa.

A. Kwanza tunafaa kuhakikishi kama mwandishi alitumia lugha ya kawaida. Kanuni hii inapaswa kuzingatiwa katika Biblai yote. Soma kifungu na kukichukulia kwa lugha ya kawaida.

B. Jinsi tunavyokichukua kifungu inapaswa kuwa kwa njia ya mfano ikiwa maneno au kifungu kikitafsiriwa katika kugha ya kawaida kinaleta maana. Isaya 55:12, ni mfano mzuri. Milima haitaimba au miti kupiga makofi. Kile ambacho mwandishi anataka kueleza ni kwamba kutakuwa na kushangilia kwa ajabu.

C. Tunapaswa kuchambua kwanza maandishi ya nabii ndipo tuyatasfiri.

i. Mara kwa mara ujumbe wa manabii ulihusu kutotii kwa watu na adhabu amabyo walikuwa wanaenda kupata. Mara kwa mara pia kulikuwa na mwito wa toba na msamaha. Lakini pia kulikuwa na wakati aliachilia adhabu.

ii. Kuna unabii ambao ulihusu maisha ya mbeleni. Leo 1% moja ya unabii ambayo haijatumika. Unabii mwingi umetimia.

iii. Tunapaswa kufahamu historian a tamaduni ya mwandishi. Je, nabii alimfundishi nani?

iv. Msingi wa ujumbe wa manabii ulikuwa kwa watu wa wakati huo. Mara kwa mara nabii aliwaonya watu kwamba walikuwa wanatenda dhambi na Mungu angewahukumu ikiwa hawangetubu na kubadilika na kumgeukia Mungu. Haya yalikuwa mafundisho.

4. Mashairi ya kiyahudi- kitabu cha Ayubu, Zaburi, Mitahli, Mhubiri na WSimbo uliyo Bora.

- A. Sehemu kubwa ya Agano la Kale imeandikwa kwa njia ya mashairi. Kwa sababu ni jambo la Muhimu sana kwa wanaotafsiri na wahubiri kufahamu Mashairi ya kiyahudi. Katika mashairi mambo huwa yanarudiwa rudiwa. Kufafanisha jambo au mambo ni jambo ambalo linafanyika bila kupoteza maana ya kifungu.
- B. Aina ya mashairi.

i. Kufanisha ni kuweka mambo pamoja na jambo hili linajidhihirisha kwa njia tofauti tofauti kama katika Zaburi 3:1-2.

ii. Usawa: hapa mambo ambayo yanazingatiwa ni sawa (Zaburi 25:4).

iii. Kujengwa: wazo moja linakamiliha la kwanza (Zaburi 23:1).

iv. Kuondoa: wazo la kwanza ni kinyume na la kwanza (Zaburi 1:6).

- C. Mashairi yanaandikwa na kusudi la kumpa msomaji mifano ambayo inakamilishwa na mafumbo.

i. Mfano ni fumbo. Huwa ni maneno ambayo yanatumika kuoneysha jambo mambo. Huwa neno linatolewa katika maana yake ya kwanza na kutumika kumaanisha jambo lingine.

"Nilimpiga kwa fimbo- kumaanisha kupiga.

"Nilimshinda katika mabishano; kumaanisha kushinda. Huwa tunatumia mifano kulinganisha bila kutumia neno "kama," kwa sababu huwa utakuwa msemo. Msemo ni kufafanisha wazi na kingine. Kwa mfano "Jane ni kama mtoto.

D. Msemo huwa unaonyesha kwamba kitu kimoja ni kama kingine. Mfano unaonyesha kwamba kitu kimoja kinafafa na kingine. Msemo, "wanadamu wote ni kama nyasi (1 Petro 1:24). Mfano ni, kila mwanadamu ni nyasi (Isaya 40:6). Hii ndio tofauti ya mambo haya mawili. Mfano mara huwa si wa kweli kama msemo. Msemo unasema kama kondoo na mfano unasema kwamba sisi ndio kondoo wa malisho.

- E. Kwa ajili ya kusisitiza, kuna mistari ambayo imerudiwa (Zaburi 6:6).

F. Miongozo ya mashairi ya kiebrania ni kutafsiri kulingana na mazingira. Kuwa mwangalifu kwa viasharia ambavyo vinasaidia kugawanya Zaburi katika vitengo vya kuwazia. Tathmini mistari ya mashairi ambayo yanajumlisha sehemu ya kuwazia ili uweze kuamua ile ambayo inafaa.

VII. Kutafsiri Agano Jipya

1. Mifano

- A. Mtu ambaye anapeana hadithi mzuri hatawahi kukosa wasikilizaji. Yesu alikuwa mzuri sana kwa kupeana hadithi na hadithi zake zilikusudiwa kufundisha mambo ya kiroho. 1/3 mafundisho ya Kristo kama yalivyonyukuliwa katika vitabu vya Injili, ni mifano. Mathayo aliandika kwamba Yesu alitumia mifano hii mara kwa mara (Mathayo 13:34). Watu huwa wanakumbuka hadithi nzuri.
- B. Mfano ni hadithi kuhusu maisha ambao umekusudiwa kufundisha ukweli au kujibu swali. Katika mafundisho ya Kristo, mfano ulikuwa na mafundisho zaid. Kusudi moja ilikuwa kuuficha ukweli kwa wale ambao hawatii, na kuweka wazi ukweli wale ambao wanatii. Maana halisi ya mfano ni kwa kanisa. Yesu alifanya hivi kwa kueleza hadithi kuhusu maisha ya kawadia ambayo ingefahamika vyema kabisa.
- C. Mifano huwa unahusu jambo moja. Yesu alifundisha kuhusu Ufalme wa Mungu ambao aliuelewa vyema kabisa.
- D. Kuna hatua nne za kutusaidia kufahamu mifano
 - i. Anza na mazingira ambayo umo. Je, nini mfano unafundisha?

A. Luka 15, tunasoma kuhusu hadithi ya mwana mpotevu. Je, tunafundishwa nini katika hadithi hii? Yesu alipeana mfano huu kuonyesha tofauti ya yule ndugu mkubwa ambaye hakuwa tayari kusamehe na baba ambaye alikuwa alikuwa tayari kusamehe ambaye ni mfano wa Kristo.

E. Wakati mwingine maana ya mfano inapeanwa katika jinsi tunapaswa kuishi maisha yetu kulingana na mfano huo kama katika Mathayo 24:44. Maana hapa ni kwamba ni lazima tuwe tayari kwa sababu Yesu anakuja wakato wowote.

F. Tambua mambo yasio ya muhimu. Mfano katika Luka 17:7-10 kuna sehemu ambazo si za muhimu kwa ukweli ambao unafundishwa. Dsehemu ya muhimu inafundisha kwamba hatufai kutarajia kusifiwa kwa sababu ya kufanya mema.

G. Tambua yalio ya muhimu.

i. Baba ambaye anakimbia na kumlaki mwaname katika hadithi ya mwana mpotevu, ni jambo la muhimu. Anaonyesha kwamba alikuwa anamsubiri mwanawe sana.

4. Miongo zaidi kuhusu utafsiri wa Biblia.

A. Mara kwa mara mfano umekusudiwa kufundisha jambo moja.

B. Wakati mwingine funzo linaweza kupatikana katika sehemu ya kwanza ya mfano kama Luke 18:1-8.

C. Wakati mwingine maana ya mfano inaelezwa mwisho wa mfano kama Luka 15:3-10.

D. Usitafuta maana ya kila jambo katika mfano. Hii ni kwa sababu mtu anaweza kuanza kujiwekea maana ambayo mwandishi hakusudia.

E. Hatufai kuanza kutafuta mafundisho mengine ambayo si msingi wa mfano huo. Usichukua baadhi ya mambo katika mfano na kuyafanya msingi wa mfano ikiwa hayafundishwi. Mfano unaweza kuchangia katika mafundisho fulani, lakini tukumbuke mafundisho muhimu ya Biblia lazima yatoka katika vifungu halisi. Kwa mfano Mathayo 25, ambapo tunasoma kuhusu hadithi ya wanawali kumi na wawili. Mfano huu haufundishi mafundisho ya msingi yoyote. Tunafundishwa kwamba tunapaswa kuwa tayari kila wakati kuwa tayari kwa ajili ya kurudi kwa Kristo. Mafundisho haya pia yanapatikana katika Matendo 1:11; Yohana 14:3, na Ufunuo 1:7.

VII. Muhtasari wa masomo haya

1 Mafundisho mengi ya Biblia yanapaswa kufahamika jinsi yameandikwa. Mafundisho ya msingi yako wazi kabisa na yanarudiwa rudiwa ili tusikose kufahamu ujumbe wa Biblia.

2. Tumia mantiki kufahamu vifungu fulani.

A. Hatua tofauti za uchanbuzi wa maandishi yanafuatana na kila hatua inajenga juu ya matokeo ya kifungu ambacho kimemalizika hadi ujumbe wa kifungu chote ufahamike.

Hatua hizi zinaendelea kwamba moja inakuleta karibu na kufahamu ukweli wa kifungu.

Ili kufikia muhtasari wa kifungu, msomaji anatakikana kutumia mbinu zote ambazo tumezungumzia.

i. Kwa mfano, Wakolosai 1:21-23, tunaona hatua ambazo zimechukuliwa kama zifuatazo:

Wakolosai walikuwa wamepotea kwa sababu ya dhambi.

Wakolosai waliokolewa kwa sababu ya kifo cha Kristo.

Wakolosai Mungu aliwaona kuwa watakatifu kwa sababu ya kazi ya Kristo.

3. Je, utafsiri wangu unakubaliana na maandiko mengine ya Biblia? Kumbuka kwamba utafsiri wako unapaswa kukubaliana na Biblia kwa sababu Biblia huwa haipingi Biblia. Tumia Biblia kupata utafsiri mzuri. Biblia inaelewana. Ikiwa msomaji atajieleza kwamba Biblia haielewani, ni wazi kwamba ni yeye ambaye atakuwa na makossa mwenyewe. Tumia vifungu ambavyo vinazungumza jambo sasa kutafsiri vifungu vingine.

4. Je, utafsiri wako unakubaliana na utafsiri wa watu wengine? Kumbuka kwamba watu wanaweza kufanya makossa, lakini hata hivyo unapaswa kuona maoni yaw engine pia.

5. Soma Biblia na lengo la kubadilishwa. Usije kwa Biblia ukiwaza kwamba unajua kile ambacho Biblia inakifundisha.

A. Kwa mfano kuna watu ambao wanawaza kwamba ikiwa mtu anahudhuria kanisa fulani, Ni wazi kwamba yeye anaenza jahanum. Wanapuuza ukweli kwamba Kristo anamhukumu mtu kibnafsi.

B. Yesu alikemea kanisa la Sardis (ufunuo 3). Lakini katika mistari ya 4-5, anasema kwamba kuna wachache katika kanisa hilo ambao walikuwa waaminifu. Hii inamaana kwamba kuna wakristo katika makanisa mengi.

6. Roho Mtakatifu pekee ndiye anaweza kutusaidia kutafsiri Biblia vyema kabisa. Omba Mungu akusaidie (1 Wakorintho 2:14).

7. Kumbuka kwamba nambari za sura na mistari si baadhi ya uandishi wa Biblia halisi. Haya ni mambo ambayo yaliongezwa na wanadamu kurahihisha usomaji wa Biblia. Kwa hivyo jambo hili halifai kushawishi jinsi unavyosoma Biblia.

8. Usianze kuvumbua mafundisho ya msingi kutokana na mstari mmoja. Mafundisho kama yale ya wokovu kwa imani na wala si kwa matendo mazuri ya mwanadamu, yanafundishwa katika Biblia nzima (Yohana 3:27; 6:52-65; Wafilipi 1:29; Matendo ya Mitume 16:14, 18:27; Waefeso 2:8-10).

A. Mara kwa mara watu hutumia mstari mmoja kuhakikisha yale ambayo wanayataka. Kwa mfano:

i. Mathayo 19:12, inatumika na makanisa fulani kufundisha kwamba wachungaji wa makanisa fulani hawapaswi kuoa. Hii tafsiri ya uongo.

ii. Kuna wengi ambao wametumia Mwanzo 9:20-27, kufanya watu waesi watumwa wao. Kuna wale ambao wanasema kwamba alama ambayo iliwekwa kwa Kanani ilikuwa nyeusi. Huu pia ni uongo.

VIII. Mambo muimu

Kama uko na Biblia yenye maelezo saidi au Kamusi ya Biblia, angalia maana ya maneno. Kwa minajili ya Biblia yenye maelezo tumia viashirio yenye iko kando au chini yake ili upate mahala ambapo neno inapatikana pia. Tumia Concodansi ili upate mahala ambapo maneno inapatikana katika Biblia.

IX. Jambo la mwisho kuhusu utafsiri wa Biblia ni kuhusus usaidisi wa Mungu mwenyewe.

Umba na umwulise Mungu akusaidie ili uelewe maana ya somo. Ukingangana kuelewa maana, maana inapaki kuvichwa. Ni lazima ungangane kabisa ili uelewe yale Mungu ana nena. Kama aulewi, umba na uambie Roho Mtakatifu akusaidie ili uelewe na Mungu atakusaidie kila wakati.